

Kujizoeza kwa njia mpya ya maisha inaweza kuchukua muda. Kijitabu hiki kinanua kukusaidia kuelewa maisha katika Uskoti. Huto maelezo fupi kuhusu desturi, tabia, sheria na masharti ambayo yanaweza kuwa tofauti na ya nchi yako ya asili



Vizuio vya umri wa kisheria

Watu kwa jumla huzingatiwa kuwa wazima au wa umri wa kisheria baada ya miaka 18. Hata hivyo, umri wa kisheria kwa hali zingine unaweza kulingana kama ifuatavyo:

- Kunywa pombe – lazima uwe na **miaka 18** au zaidi
- Uvutaji sigara – lazima uwe na **miaka 18** au zaidi
- Kupata leseni ya kuendesha gari – lazima uwe na **miaka 17** au zaidi
- Kuacha shule – lazima uwe na **miaka 16** au zaidi
- Idhini ya ngono – lazima awe na **miaka 16** au zaidi ili kuwa na uhusiano wa kingono.

Watoto

- Wazazi huzingatiwa akuwajibika kwa watoto wao hadi umri wa miaka 18
- Watoto wadogo wasiachwe peke yao bila kutazamwa katika maeneo ya hadhara au hata nyumbani.
- Kuchapa watoto hakuruhusiwi

Uvutaji sigara

- Uvutaji sigara haurusiwi mahali popote unapoona ishara hii
- Uvutaji sigara hauruhusiwi katik amaeneo ya ndani au maeneo yaliyofungwa ya hadhara, ikiwa ni pamoja na ofisi, mikahawa, baa, sinema
- Uvutaji sigara katika maeneo yasiyokubalishwa kutatozwa faini
- Uvutaji wa sigara unakubalishwa nje, nyumbani mwako au katika gari lako, ila kama imeelezwa tofauti na mkabaila wako au iwapo gari lako linatumika kwa mambo ya biashara.



Pombe

- Unywaji pombe katika maeneo ya hadhara, kama vile mtaani au kwenye bustani hakuruhusiwi. Kufanya hivi kunaweza kuleta faini.

Visu

- Ubebaji wa kisu ni kinyume na sheria katika Uskoti. Iwapo umesimamishwa na polisi na umebeba kisu, kunaweza kusababisha kukamatwa.
- Visu haviruhusiwi shuleni.

Utupaji taka

- Utupaji au uangushaji taka au vitu visivyotakikana kutatoza faini ya £50.

Ubaguzi

- Ni kinyume cha sheria kuendewa, au kutendea mtu tofauti au kuwabagua kwa sababu ya umri wako, ulemavu, upangaji mbaya wa kijinsia, ndoa na ndoa ya kiserikali, mimba na uzazi, rangi, dini na imani, ngono au uelekeo wa kingono.
- Ushambulizi ni kinyume cha sheria na unaweza kusababisha kushtakiwa
- Iwapo unahisi kama umeshambuliwa, kwa maneno au au kimwili, unapaswa kuwasiliana na polisi. Unaweza pia kupata usaidizi kwa kuongea na mtu katika Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti au kuwasiliana na Kikosi Maalum cha Tabia Zinazopingana na Jamii katika 0800 027 3901

Uhasama dhidi ya wanawake

- Uhasama dhidi ya wanawake inaweza kuwa pamoja na dhuluma za kinyumbani, ubakaji, uvamizi wa kijinsia, ukahaba, utumiaji vibaya wa kijinsia na uuzaji haramu, dhuluma ya kingono kwa watoto, utahirishaji wa wasichana (FGM), ndoa ya lazima na uhalifu wa heshima
- Wanawake wote na wasichana katika Uskoti wana haki ya kisheria ya kutofanyiwa aina yoyote ushambulizi dhidi ya wanawake
- Dhuluma za nyumbani ni pamoja na dhuluma za kimwili, za kingono, za kisaikolojia na za kifedha
- Usaidizi wa kisiri unapatikana kwa yeyote anayepitia aina yoyote ya vurugu au dhuluma za nyumbani

Usaidizi na ushauri unapatikana kwa mashirika kama vile:

- Simu ya Usaidizi ya Dhuluma za Kinyumbani dhidi ya Wanawake wa Uskoti: 0800 027 1234 (masaa24)
- Simu ya Kitaifa ya Usaidizi Dhidi ya Ushambulizi wa Kijinsia na Ubakaji: 08088 01 03 02
- Archway Glasgow: 0141 211 8175

Tofauti katika desturi na tabia zinazokubalika

Hata kama tabia zingine hazijakingwa na sheria, desturi za Uskoti na matarajio yanaweza kuwa tofauti na ya nchi yako ya asili. Haya yanaweza kuwa pamoja na:

- Matarajio kuhusu nafasi binafsi na mawasiliano ya kibinafsi hulingana na nchi. Katika Uingereza watu hutarajia kupewa nafasi yao katika uhadhara ili kuweza kuhisi kustareheka
- Mikusanyiko kwa vikundi vikubwa, hasa vya vijana, vinaweza kuonekana kama za kuogofya.
- Njia ya kawaida ya kusalimia wanawake na wanaume katika Uingereza ni kusema 'habari' na/au kupeana mkono

Uendeshaji katika Uingereza

Iwapo umetuma ombi la utafutaji kimbilio katika Uingereza na hujapokea haki ya kubakia, hutaweza kutuma ombi la leseni ya uendeshaji gari ya Uingereza kuanzia Machi 25, 2010.

Iwapo una ufikiaji halali wa gari lazima uwe na:

- Leseni halali ya kuendesha gari
- Bima ya gari
- Hati halali ya kuthibitisha kuwa gari yako iko sawa
- Diski halali ya ushuru ya barabara
- Iwapo una leseni halali ya uendeshaji gari kutoke nchi ya nje ya Uingereza na thibitisho la nyaraka la hii, utaweza kuendesha na leseni yako ya ng'ambo hadi miezi 12 kutoka tarehe uliyoingia Uingereza.
- Unaweza kushtakiwa kisheria iwapo unaendesha gari ukiwa chini ya ushawishi wa pobe au au dawa za kulevya

Leseni za Televisheni

- Iwapo una televisheni lazima ununue leseni yake.
- Unaweza kununua leseni ya Televisheni kwa kupiga simu **0300 790 6131**, mtandaoni katika www.tvlicensing.co.uk au kwa binafsi katika duka lolote lenye ishara hii:

